# MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Device Authority



# TAARIFA YA UTENDAJI KAZI

# 2018/2019

## Dhima

Kulinda afya ya jamii kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba

## Dira

Kuwa Mamlaka inayoongoza barani Afrika katika kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa wote.

## Falsafa

Kutoa huduma za udhibiti katika kulinda afya ya jamii na mazingira kwa kutumia wafanyakazi wenye ujuzi na ari ya kazi.

## Misingi ya kazi

- Kufanya kazi kwa ushirikiano
- Uaminifu
- Kuzingatia mahitaji ya wateja
- Ubora
- Uwajibikaji



Mhe.Ummy A. Mwalimu (MB),
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba
S.L.P 743,
11478 Dodoma.



Dkt. Zainabu Chaula,
Katibu Mkuu (Afya),
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii
Jinsia, Wazee na Watoto,
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
S.L.P 7433,
11478 Dodoma.

**Mhe. Waziri,**

Ninayo heshima kubwa kuwasilisha kwako Taarifa ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwa kipindi cha mwaka 2018/19.
Taarifa hii imeeleza utekelezaji wa shughuli za Mamlaka katika kutimiza lengo lake kuu la Kulinda Afya ya Jamii chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.
Nawasilisha.



**Dkt. Zainabu Chaula**
**Katibu Mkuu (Afya)**

# MAELEZO YA MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI (MAB)



Taarifa ya utendaji kazi kwa mwaka wa fedha 2018/19 inaainisha kazi na majukumu yaliyotekelezwa pamoja na maeneo yanayohitaji kupewa kupaumbele ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kwa sasa TMDA inatekeleza Mpango mkakati wake wa miaka mitano (5) 2017/18 - 2020/21 wa iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ambao umelenga kuimarisha utekelezaji wa jukumu la msingi la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.

Katika kipindi hiki TFDA ilitangazwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kufikia hatua ya tatu (Maturity Level Three) kwa kuwa na mifumo bora ya udhibiti wa usalama ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. TFDA imekuwa taasisi ya kwanza ya udhibiti wa bidhaa barani Afrika kufikia hatua hii.
Mamlaka imeendelea Kuboresha huduma zake kwa wateja kwa kutumia TEHAMA na kutekeleza mifumo bora ya Utendaji Kazi (Quality Management System) kwa kiwango cha kimataifa cha ISO 9001:2015 katika kutoa huduma. Aidha, Mamlaka imeendelea kuzingatia viwango vya utoaji huduma vilivyoainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja (CSC) 2016 ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja.

Taasisi imeendelea kuwekeza katika ununuzi wa vifaa vya kisasa pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa maabara. Maabara ya Chakula na ya Maikrobiolojia zimeendelea kushikilia cheti cha ithibati (accreditation) kwa kiwango cha Kimataifa cha ISO/IEC 17025:2015 baada ya kukaguliwa tena (surveillance) na taasisi za ithibati za SADCAS/SANNAS. Hii inafanya matokeo ya chunguzi zinazofanywa na maabara za TFDA kutambuliwa kimataifa.

Matumizi na usimamizi wa rasilimali za Mamlaka pamoja na utoaji huduma umeendelea kuzingatia mifumo bora ya kiutendaji, Sheria, Kanuni na taratibu ambapo hesabu za fedha na rasilimali za TFDA kwa kipindi kinachoishia Juni, 2019 zipo tayari kwa ukaguzi unaofanywa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Naipongeza Menejimenti pamoja na wafanyakazi wote wa iliyokuwa TFDA kwa kufanya kazi kwa weledi na kujituma katika kuhakikisha kuwa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi katika soko ni bora, salama na fanisi. Vilevile, natoa shukrani kwa wadau wote wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na jamii kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika kusaidia Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, natoa wito kwa wadau wote wa TFDA na wananchi kwa ujumla kutekeleza wajibu wao ipasavyo katika kuhakikisha kuwa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko vinakidhi vigezo vya ubora na usalama.

Bodi ya Ushauri (MAB) chini ya uenyekiti wangu itaendelea kutoa maelekezo kwa Menejimenti ya TMDA sanjari na ushauri kwa Wizara katika kuwahakikishia kuwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko la Tanzania ni salama, bora na vyenye ufanisi.

**Balozi Dkt. Ben Moses**
**MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI**

# MAELEZO YA MKURUGENZI MKUU



Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) hivi sasa inajulikana kama Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 2019 yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019 iliyoanza kutekelezwa tarehe 1 julai, 2019 ambapo jukumu la kudhibiti chakula na vipodozi limehamishiwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS). TMDA inajukumu la kudhibiti dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini.
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inatekeleza majukumu yake chini ya Mpango Mkakati wa iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).
Taarifa ya utendaji kazi ya TFDA kwa mwaka wa fedha 2018/19 inaainisha majukumu na kazi zilizofanyika katika kipindi tajwa. Aidha, changamoto zilizojitokeza pamoja na mbinu zilizotumika katika kukabiliana na changamoto hizo zimeanishwa.
Huu ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa mpango mkakati wa TFDA wa awamu ya nne wenye miaka mitano (2017/18-2021/22) ambapo mafanikio makubwa yameonekana. Jumla ya maombi 1,305 ya dawa za binadamu yalipokelewa na 1,182 kati ya hayo sawa na 91% yalitathminiwa ambapo 690 (58%) yaliidhinishwa. Aidha, maombi 115 ya dawa za mifugo yalipokelewa na 88 kati ya hayo (77%) yalifanyiwa kazi na 86 sawa na 98% yalikidhi vigezo na kuidhinishwa.
Mamlaka pia ilipokea jumla ya maombi 2,196 ya vipodozi na yote (100%) yalitathminiwa na kati ya hayo 2,156 (98%) yaliidhinishwa. Vile vile, Maombi 357 ya usajili wa vifaa tiba yalipokelewa na kati ya hayo 325 (91%) kufanyiwa kazi ambapo maombi 92 (28%) tu yaliidhinishwa. Uchache wa maombi yaliyoidhinishwa ulitokana pamoja na mambo mengine kutojitosheleza kwa taarifa za kisayansi za baadhi ya vifaa tiba husika.
Aidha, maombi 4,349 (99%) ya usajili wa maeneo ya biashara kati ya 4,390 yaliyokuwepo yalifanyiwa kazi ambapo maeneo 4,275 (98%) yalisajiliwa.

Vilevile, Mamlaka ilipokea maombi 3,353 ya usajili wa bidhaa za chakula ambapo yote (100%) yalifanyiwa tathmini. Maombi 2,876 (86%) kati ya yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa. Idadi ya maombi ya usajili yaliyoidhinishwa imeongezeka kutoka

2,104 mwaka 2017/18 hadi kufikia 2,876 kwa mwaka 2018/19 ikiwa ni ongezeko la maombi 772. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa shughuli za udhibiti na utii wa sheria bila shuruti miongoni mwa wafanyabiashara.

Aidha, jumla ya maombi 6,356 ya usajili wa maeneo ya biashara ya chakula yalipokelewa katika kipindi tajwa ambapo 6,325 (99.5%) yalifanyiwa kazi na kati ya hayo maeneo 5,955 (94%) yalikidhi vigezo na kusajiliwa. Vile vile, maeneo 10,055 yanayojihusisha na biashara ya chakula yalikaguliwa ambapo maeneo 7,818 (78%) yalikidhi vigezo.

Idadi ya maeneo yaliyokidhi vigezo na kuidhinishwa kwa mwaka 2018/19 yameongezeka kwa maeneo 725 ikilinganishwa na maeneo 7,092 yaliyokidhi vigezo mwaka 2017/18. Wastani wa kukidhi vigezo kwa maeneo yaliyokaguliwa umeongezeka kutoka 69% kwa mwaka 2017/18 hadi 78% kwa kipindi hiki. Ongezeko hili limechangiwa na ushirikiano walioupata wadau wa chakula kutoka kwa wakaguzi, vitendea kazi na uelewa kwa wateja.

Mamlaka pia ilipokea maombi 8,533 ya kuingiza bidhaa za chakula nchini na 8,447 kati ya hayo yalikidhi vigezo na kutolewa vibali. Maombi 2,524 ya kusafirisha chakula nje ya nchi yalipokelewa na kati ya hayo 2,502 yalipatiwa vibali.

Katika mwaka huu wa fedha jumla ya sampuli 5,067 zilipokelewa katika maabara za TFDA na sampuli zote (100%) zilichunguzwa na 4,580 (90%) zilifaulu. Aidha, katika kuhakikisha kwamba viwango vya ISO / IEC 17025:2005 na WHO/GLP vinafuatwa na kutekelezwa, Mamlaka ilikaguliwa na bodi ya ithibati SADCAS/SANAS Kwenye maabara za Chakula pamoja na Maikrobailojia na kufaulu, hivyo kuendelea kushikilia cheti hicho cha ithibati.

Elimu kwa umma ilitolewa kwa makundi mbalimbali ya wananchi pamoja na kutangaza huduma za Mamlaka kupitia njia mbalimbali za uelimishaji. Njia zilizotumika ni pamoja na kufanya mihadhara (Outreach Campaigns) 58 ambapo Zaidi ya watu 39,073 walifikiwa, kurusha matangazo mafupi ya uelimishaji kupitia vituo vinne vya runinga na redio na kushiriki katika maonesho mbali mbali.

Kwa upande wa usimamizi wa rasilimali, Jumla ya TZS 52.1 bilioni zilikusanywa sawa na 98% ya bajeti ya makusanyo ya TZS 53.3 billoni ya mwaka 2018/2019. Kati ya hizo TZS 47.9 (92%) ni ada na tozo, TZS 4 bilioni sawa na (7.7%) ni mchango wa Serikali kuu na TZS 116 milioni (0.3%) ni fedha za Washirika wa Maendeleo. Mamlaka ilitumia jumla ya TZS 45 bilioni sawa na 81% ya bajeti iliyopangwa mwaka huu 2018/19 ambayo ni TZS 53 bilioni katika kuendesha taasisi.

Mfumo wa IMIS umeboreshwa pamoja na TFDA kuunganishwa na mfumo wa malipo wa Serikali na hivyo kuwezesha wateja kufanya malipo kwa kutumia namba maalum (Control Number) kupitia benki zilizounganishwa katika mfumo huu.

Kwa ujumla TFDA ilitekeleza Malengo Mkakati ya kwa ufanisi na mafanikio na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza watumishi wote wa iliyokuwa TFDA kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwaomba wazidi kuwa na ari na moyo wa kazi. Aidha, shukrani za dhati kwa Mwenyekiti na wajumbe wa bodi kwa maelekezo yao kipindi chote cha mwaka 2018/19.

**Adam M. Fimbo**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

# TAARIFA YA UTENDAJI KAZI YA MWAKA 2018/19

## 1. UTANGULIZI

Taarifa hii inaainisha kazi zilizotekelezwa na TFDA kwa kipindi cha mwaka 2018/19 kwa kuzingatia Mpango kazi na Bajeti ulioidhinishwa. Utekelezaji wa majukumu haya umezingatia malengo mkakati nane (8) kama yalivyo katika Mpango Mkakati wa TFDA (2017/18 - 2021/22) ambapo huu ni mwaka wa pili (2) wa utekelezaji wake. Malengo ya Mpango Mkakati wa Mamlaka ni haya yafuatayo:-

i) Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi;
ii) Kuhakikisha usalama na ubora wa chakula;
iii) Kuboresha huduma za maabara;
iv) Kuimarisha utoaji elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa wateja;
v) Kuimarisha uwezo wa Mamlaka katika kutoa huduma za kiudhibiti;
vi) Kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kuboresha huduma kwa waathirika wa UKIMWI na wenye magonjwa yasiyoambukiza;
vii) Kuimarisha na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa; na
viii)Kuboresha masuala ya jinsia na mazingira.

## 2. HATUA YA UTEKELEZAJI WA KILA LENGO MKAKATI

TFDA imetekeleza kazi katika kipindi cha mwaka 2018/19 kwa mujibu wa mpango kazi na bajeti ya 2018/19 ili kufikia lengo la kila Mpango Mkakati. Kazi zilizotekelezwa kwa kila lengo ni kama ilivyoainishwa katika vipengele 2.1 - 2.6.

### 2.1 KUHAKIKISHA USALAMA, UBORA NA UFANISI WA DAWA, VIPODOZI, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

Mamlaka ina jukumu la kulinda afya za wananchi dhidi ya athari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi. Hii ni pamoja na kufanya usajili na ukaguzi wa bidhaa husika, kufuatilia madhara yatokanayo na dawa, vipodozi na vifaa tiba; na kufuatilia ubora na usalama wa bidhaa hizo katika soko. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Mamlaka ilitekeleza kazi zifuatazo:-

#### 2.1.1 Usajili wa dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi

Kabla ya bidhaa kusajiliwa na kuruhusiwa kuingia katika soko, ni lazima ifanyiwe tathmini za kisayansi ili kuthibitisha usalama, ubora na ufanisi wake. Baada ya kufanyiwa tathmini kwa kuzingatia Kanuni, Miongozo na Viwango vya Kitaifa na kimataifa ndipo usajili wa bidhaa husika hufanyika. Matokeo ya tathmini na usajili wa bidhaa za dawa za binadamu na mifugo, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi yameainishwa katika kipengele 2.1.1.1 hadi 2.1.1.8 na mchanganuo wake umeoneshwa katika majedwali 1(a), (b) na (c).

##### 2.1.1.1 Tathmini na usajili wa dawa za binadamu

Mamlaka ilipokea maombi 1,305 ambapo maombi 1,182 (91%) kati ya hayo yalifanyiwa tathmini na maombi 690 (58%) ya yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa na bidhaa hizo kusajiliwa. Maombi mawili (2) yalikataliwa



kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1(a).

Vile vile, kulikuwa na jumla ya maombi 2,135 yanayohusu mabadiliko na majibu ya hoja za usajili wa dawa za binadamu ambapo 1,975 (93%) yalitathminiwa na 904 (46%) ya yaliyotathminiwa yaliidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali na 1(b).

**2.1.1.2 Tathmini na usajili wa dawa za mifugo**

Katika kipindi hiki, kulikuwa na jumla ya maombi 115 ya usajili wa dawa za mifugo ambapo maombi 88 (76%) yalifanyiwa tathmini. Maombi 86 kati ya yaliyofanyiwa tathmini yalisajiliwa. Mchanganuo wa maombi hayo umeainishwa kwenye Jedwali Na. 1(a).

Aidha, kulikuwa na maombi mengine 93 yanayohusu mabadiliko na majibu ya hoja za usajili wa dawa za mifugo ambapo maombi yote yalifanyiwa tathmini na maombi 13 (14%) yaliidhinishwa kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 1(b).

**2.1.1.3 Tathmini na usajili wa dawa za mitishamba**

Maombi tisa (9) ya dawa za mitishamba yalipokelewa na kufanyiwa tathmini ambapo maombi sita (6) yaliidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali Na. 1(a). Aidha, maombi mengine nane (8) ya mabadiliko ya usajili wa dawa za mitishamba yalipokelewa na yote yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 1(b).

**2.1.1.4 Tathmini na usajili wa vipukusi**

Mamlaka ilipokea maombi 43 mapya ya vipukusi ambapo maombi 41 (95%) yalifanyiwa tathmini na kati ya hayo maombi 45 (110%) yaliidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali Na. 1(a). Idadi ya maombi yaliyoidhinishwa ni kubwa kuliko yaliyofanyiwa tathmini kwa sababu baadhi ya maombi yaliyotathminiwa katika kipindi cha mwisho wa mwaka 2017/18 yaliidhinishwa ndani ya kipindi cha mwaka 2018/19.
Vile vile majibu ya hoja 10 za vipukusi yalipokelewa na yote yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye jedwali Na. 1(b).

**2.1.1.5 Tathmini na usajili wa vipodozi**

Jumla ya maombi 2,196 ya usajili wa vipodozi yalipokelewa na yote kufanyiwa tathmini. Maombi 2,162 (98%) yaliyokidhi matakwa ya usajili yaliidhinishwa. Maombi 30 ya usajili wa vipodozi yalikataliwa kwa kuwa hayakukidhi matakwa ya usajili.

Aidha maombi mengine 238 ya vipodozi yanayohusu matangazo, mabadiliko na majibu ya hoja za usajili wa vipodozi yalipokelewa. Maombi yote yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 105 (100%) ya matangazo na mabadiliko yaliidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali 1(b).

**2.1.1.6 Tathmini na usajili wa vifaa tiba**

Mamlaka ilitathmini maombi 325 (91%) kati ya maombi 357 ya usajili wa vifaa tiba yaliyopokelewa. Maombi 92 (28%) ya yaliyofanyiwa tathmini yalikidhi vigezo na kuidhinishwa. Mchanganuo wa maombi haya umeoneshwa katika Jedwali Na. 1(a).

Vile vile maombi mengine 121 yanayohusu mabadiliko na majibu ya hoja za usajili wa vifaa tiba yalipokelewa ambapo maombi 104 (86%) yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye jedwali 1(b).

**2.1.1.7 Tathmini na usajili wa vitendanishi**

Maombi 171 ya usajili wa vitendanishi yalipokelewa na kati ya hayo, maombi 145 (85%) yalifanyiwa tathmini na maombi 23 yalisajiliwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali 1(a). Vile vile maombi mengine 35 ya majibu ya hoja yalipokelewa ambapo maombi 32 (91%) kati ya hayo yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye jedwali 1(b).

**2.1.1.8 Tathmini ya maombi ya majaribio ya dawa**

Maombi 16 ya majaribio ya dawa yalipokelewa na kati ya hayo, maombi 14 (88%) yalifanyiwa tathmini na maombi 9 (64%) kati ya yaliyotathminiwa yaliidhinishwa kama ilivyoanishwa kwenye jedwali 1(a). Aidha, maombi mengine 35 ya majibu ya hoja na mabadiliko yalipokelewa ambapo yote yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye jedwali 1(b).
Jedwali 1 (a): Idadi ya maombi ya usajili wa bidhaa za dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi

| Aina ya bidhaa | | Maelezo | Baki ya 30 June 2018 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Hoja | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dawa | Binadamu | Mapya | 67 | 688 | **755** | 669 | 286 | 2 | N/A | **86** |
| | | Huisha | 46 | 504 | **550** | 513 | 404 | 0 | N/A | **37** |
| | | **Jumla ndogo** | **113** | **1,192** | **1,305** | **1,182** | **690** | **2** | N/A | **123** |
| | Mifugo | Mapya | 5 | 48 | **53** | 41 | 44 | 0 | N/A | **12** |
| | | Huishwa | 0 | 62 | **62** | 47 | 42 | 0 | N/A | **15** |
| | | **Jumla ndogo** | **5** | **110** | **115** | **88** | **86** | 0 | N/A | **27** |
| | Mitishamba | Mapya | 0 | 9 | 9 | 9 | 6 | 0 | N/A | **0** |
| | | **Jumla ndogo** | **0** | **9** | **9** | **9** | **6** | **0** | N/A | **0** |
| Majaribio ya dawa | | Mapya | 0 | 16 | 16 | 14 | 9 | 0 | 7 | **2** |
| | | **Jumla** | **0** | **16** | **16** | **14** | **9** | **0** | **7** | **2** |
| Vipodozi | | Mapya | 0 | 1,810 | 1,810 | 1,810 | 1,776 | 34 | N/A | **0** |
| | | Huishwa | 0 | 386 | 386 | 386 | 386 | 0 | N/A | **0** |
| | | **Jumla ndogo** | **0** | **2,196** | **2,196** | **2,196** | **2,162** | **30** | **N/A** | **0** |
| Vipukusi (*Antiseptics* na *Disinfectants*) | | Mapya | 0 | 43 | **43** | 41 | 45* | 3 | N/A | **2** |
| | | **Jumla ndogo** | **0** | **43** | **43** | **41** | **45** | **3** | **N/A** | **2** |
| Vifaa tiba | | Mapya | 72 | 280 | 352 | 325 | 92 | 0 | 233 | **27** |
| | | Huishwa | 0 | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | **5** |
| | | **Jumla ndogo** | **72** | **285** | **357** | **325** | **92** | **0** | **233** | **32** |
| Vitendanishi | | Mapya | 0 | 171 | 171 | 145 | 23 | 0 | 117 | **26** |
| | | **Jumla ndogo** | **0** | **171** | **171** | **145** | **23** | **0** | **117** | **26** |
| **Jumla Kuu** | | | **190** | **4,022** | **4,212** | **4,000** | **3,117** | **39** | **357** | **208** |

***Idadi inajumuisha maombi yaliyopokelewa katika kipindi cha nyuma**

**Jedwali 1(b): Mchanganuo wa maombi mengine yanayohusu usajili wa bidhaa**

| Na | Aina ya bidhaa | | | Maelezo | Baki 2017/18 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dawa | Binadamu | | Matangazo | 100 | 393 | 493 | 448 | 285 | 4 | 45 |
| | | | | Mabadiliko | 23 | 751 | 774 | 664 | 619 | 2 | 110 |
| | | | | Majibu ya Hoja | 33 | 835 | 868 | 863 | 0 | 2 | 0 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **156** | **1,979** | **2,135** | **1,975** | **904** | **8** | **155** |
| | | Mifugo | | Mabadiliko | 0 | 19 | 19 | 19 | 13 | 0 | 0 |
| | | | | Majibu ya Hoja | 1 | 73 | 74 | 74 | 0 | 0 | 0 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **1** | **92** | **93** | **93** | **13** | **0** | **0** |
| | | Mitishamba | | Majibu ya Hoja | 0 | 8 | 8 | 8 | 0 | 0 | 0 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **0** | **8** | **8** | **8** | **0** | **0** | **0** |
| | Majaribio ya dawa | | | Mabadiliko | 0 | 21 | 21 | 21 | 21 | 0 | 0 |
| | | | | Majibu ya Hoja | 0 | 14 | 14 | 14 | 14 | 0 | 0 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **0** | **35** | **35** | **35** | **35** | **0** | **0** |
| 2 | Vipodozi | | | Matangazo | 0 | 26 | 26 | 26 | 26 | 0 | 0 |
| | | | | Mabadiliko | 0 | 79 | 79 | 79 | 79 | 0 | 0 |
| | | | | Majibu ya Hoja | 0 | 133 | 133 | 133 | N/A | N/A | 0 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **0** | **238** | **238** | **238** | **105** | **0** | **0** |
| 3 | Vifaa tiba | | | Mabadiliko | 0 | 13 | 13 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| | | | | Majibu ya Hoja | 0 | 108 | 108 | 104 | N/A | N/A | 4 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **0** | **121** | **121** | **104** | **0** | **0** | **17** |
| 4 | Vitendanishi | | | Majibu ya Hoja | 0 | 35 | 35 | 32 | N/A | N/A | 3 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **0** | **35** | **35** | **32** | **0** | **0** | **3** |
| 5 | Vipukusi | | | Majibu ya Hoja | 0 | 10 | 10 | 10 | 0 | 0 | 0 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **0** | **10** | **10** | **10** | **0** | **0** | **0** |
| | **Jumla Kuu** | | | | **157** | **2,518** | **2,675** | **2,495** | **1,057** | **8** | **175** |

**N/A- Not applicable**

(MHW)

2.1.1.10 Maombi ya usajili wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ambayo hayajafanyiwa tathmini kulingana Mkataba wa Huduma kwa Wateja

Kulingana na muda ulioainishwa kwenye MHW, jumla ya maombi 153 yalikuwa bado hayajafanyiwa tathmini

**Jedwali Na. 1(c): Mchanganuo wa maombi ya usajili wa bidhaa ambayo hayajatathminiwa (Age analysis)**

| Na | Aina ya Bidhaa | Idadi ya siku kwa mujibu wa *MHW** | Muda uliopita tangu maombi kupokelewa | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ≤50 | 51 - 100 | 101 - 120 | 121-200 | 201 - 250 | 251 - 300 | 301-360 | >360 | JUMLA |
| 1 | Dawa za binadamu na mifugo zinazotengenezwa nchini | **120** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 2 | Dawa za binadamu na mifugo zinazotengenezwa nchi za nje | **240** | 70 | 20 | 8* | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 98 |
| 3 | Vipukusi | **200** | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 4 | Vipodozi | **50** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Vifaa Tiba –Class A | **100** | 6 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| | Vifaa Tiba –Class B, C & D | **200** | 9 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 |
| 6 | Vitendanishi | **200** | 17 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 |
| | **JUMLA KUU** | | **104** | **41** | **8** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **153** |

**MHW* = Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa mwaka 2016**

Jedwali Na.1 (c) linaonesha kuwa jumla ya maombi 153 yalikuwa bado hayajafanyiwa tathmini hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019. Maombi hayo mengi yalipokelewa miezi miwili kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2018/2019 na kwa kipindi hicho tathmini ya maombi ya majibu ya hoja na mabadiliko ilikuwa imepewa kipaumbele. Hata hivyo, maombi yote yapo ndani ya muda wa kufanyia kazi kwa mujibu wa MHW na tathmini yake itakamilishwa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020.

### 2.1.2 Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara za dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi

Mfumo wa usajili wa maeneo ya biashara za bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza husaidia kuhakikisha kuwa maeneo husika yanakidhi vigezo ili kutoathiri usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa tajwa. Jedwali Na.2 linaonesha mchanganuo wa usajili wa maeneo ya biashara.

**Jedwali Na. 2: Maombi ya usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara za dawa, vipodozi, vifaa tiba na vipukusi**

| Na | Aina ya jengo | | | Baki kutoka mwaka 2017/18 | Yaliyopokelewa | | Jumla | Tathminiwa | Yaliyosajiliwa | Vibali vilivyotolewa | Hoja | (%) yaliyokidhi vigezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Mapya | Huisha | | | | | | |
| 1 | Dawa | Viwanda vya ndani | Vikubwa | - | - | 8 | **8** | 8 | 8 | 8 | - | 100.0 |
| | | | Kati | - | - | 4 | **4** | 4 | 4 | 4 | - | 100.0 |
| | | | Vidogo | - | 1 | 3 | **4** | 4 | 4 | 4 | - | 100.0 |
| | | Maghala | | 1 | 10 | 22 | **33** | 33 | 32 | 32 | 1 | 97.0 |
| | | Duka la jumla la dawa (Binadamu) | | 6 | 123 | 78 | **207** | 207 | 206 | 206 | 1 | 99.5 |
| | | Duka la jumla la dawa (Mifugo) | | 2 | 43 | 85 | **130** | 128 | 127 | 127 | 1 | 99.2 |
| | | DLDM Mifugo | | 1 | 91 | 147 | **239** | 219 | 218 | 217 | 1 | 99.5 |
| | | Famasi - Mifugo | | - | 7 | 11 | **18** | 18 | 18 | 18 | - | 100.0 |
| | | Magari | | 3 | 32 | 25 | **60** | 60 | 56 | 56 | 4 | 93.3 |
| | | **Jumla ndogo** | | **13** | **307** | **383** | **703** | **681** | **673** | **672** | **8** | 98.8 |

| Na | Aina ya jengo | | | Baki kutoka mwaka 2017/18 | Yaliyopokelewa | | Jumla | Tathminiwa | Yaliyosajiliwa | Vibali vilivyotolewa | Hoja | (%) yaliyokidhi vigezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Mapya | Huisha | | | | | | |
| 2 | Vipodozi | Viwanda | Vikubwa | - | 1 | 3 | **4** | 4 | 4 | 4 | - | 100.0 |
| | | | Kati | - | 1 | 4 | **5** | 5 | 4 | 4 | 1 | 80.0 |
| | | | Vidogo | - | 25 | 6 | **31** | 31 | 24 | 24 | 7 | 77.4 |
| | | Maduka ya Jumla | | 1 | 85 | 159 | **245** | 245 | 235 | 235 | 10 | 95.9 |
| | | Maduka ya Rejareja | | 9 | 1,405 | 1,588 | **3,002** | 2,985 | 2,959 | 2,954 | 26 | 99.1 |
| | | Maghala | | - | 35 | 56 | **91** | 91 | 91 | 91 | - | 100.0 |
| | | Magari ya kubebea vipodozi | | - | 26 | 18 | **44** | 42 | 31 | 31 | 11 | 73.8 |
| | | **Jumla ndogo** | | **10** | **1,578** | **1,834** | **3,422** | **3,403** | **3,348** | **3,343** | **55** | **98.4** |
| 3 | Vipukusi | Maduka ya Jumla | | - | - | 2 | **2** | 2 | 2 | 2 | - | 100.0 |
| | | **Jumla ndogo** | | **-** | **-** | **2** | **2** | **2** | **2** | **2** | **-** | 100.0 |
| 4 | Vifaa tiba | Viwanda | vidogo | 1 | - | - | **1** | 1 | 1 | 1 | - | 100.0 |
| | | Maduka ya Jumla | | 4 | 68 | 103 | **175** | 175 | 164 | 170 | 11 | 93.7 |
| | | Maduka ya Rejareja | | - | 55 | 13 | **68** | 68 | 68 | 68 | - | 100.0 |
| | | Maghala | | - | 3 | 14 | **17** | 17 | 17 | 17 | - | 100.0 |
| | | **Jumla ndogo** | | **5** | **126** | **134** | **265** | **265** | **254** | **260** | **11** | 95.8 |
| | **JUMLA KUU** | | | **28** | **2,011** | **2,351** | **4,392** | **4,349** | **4,275** | **4,275** | **74** | **98.3** |

Kwa mujibu wa jedwali Na.2, maombi 4,349 kati ya 4,392 ya usajili wa maeneo ya biashara yalifanyiwa kazi ambapo maombi 4,275 (98%) yaliidhinishwa na maeneo husika kusajiliwa na hivyo kupewa vibali vya biashara. Idadi ya maeneo yaliyosajiliwa mwaka 2018/19 imepungua kwa maeneo 455 (10%) ikilinganishwa na maeneo 4,882 yaliyosajiliwa mwaka 2017/18.

### 2.1.3 Ukaguzi wa majaribio ya dawa, viwanda na maeneo ya biashara za dawa, vipodozi na vifaa tiba

Viwanda na maeneo ya biashara za dawa, vipodozi, vifaa tiba na bidhaa nyongeza hukaguliwa wakati wowote ili kuhakiki ubora wa majengo, mifumo ya utengenezaji na mazingira ya uzalishaji, usambazaji, uhifadhi na uuzaji ili kudhibiti ubora na



usalama wa bidhaa hizi. Mamlaka hukagua viwanda, maduka yadawa za binadamu na mifugo, hospitali, vituo vya afya, maghala, maduka ya vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi na magari ya kubeba bidhaa hizi.

Mamlaka ilikagua viwanda 127 ikiwa ni viwanda 119 vya kutengeneza dawa nje ya nchi na nane (8) vya kutengeneza dawa ndani ya nchi. Viwanda 105 sawa na asilimia 83 ya viwanda vilivyokaguliwa viliidhinishwa kama ilivyoanishwa kwenye jedwali Na. 3. Aidha Mamlaka ilikagua viwanda 27 vya kutengeneza vifaa tiba vikiwemo 20 vya nje ya nchi na saba (7) vya ndani ya nchi. Viwanda 13 sawa na asilimia 65 ya viwanda vilivyokaguliwa viliidhinishwa kama ilivyoanishwa kwenye jedwali Na. 3.

Vile vile, tathmini ya maombi ya ukaguzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba(GMP Desk Review) ilifanyika ambapo Mamlaka iliandaa taratibu sanifu za kufanya kazi hii na muundo wa taarifa ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya maombi 51 (37 viwanda vya dawa) na (14 viwanda vya vifaa tiba).

Aidha, ukaguzi wa majaribio ya dawa ulifanyika kwa vituo 24 vya majaribio ya dawa katika mikoa ya Lindi (1) Morogoro (1), Pwani (5), Kilimanjaro (6), Manyara (1) na Tanga (2) na Dar es Salaam (8).

**Jedwali Na. 3: Ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara za dawa, vipodozi na vifaa tiba**

| Na | Aina ya Biashara | | Maeneo yaliyokaguliwa | | | Yaliyokidhi Vigezo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Yaliyosajiliwa** | **Yasiyosajiliwa** | **Jumla** | **Idadi** | **%** |
| 1 | Dawa | Viwanda vya nje | 119 | 0 | 119 | 104 | **87** |
| | | Viwanda vya ndani | 8 | 0 | 8 | 1 | **13** |
| | | Maghala (Binadamu) | 86 | 4 | 90 | 85 | **94** |
| | | Duka la dawa – Famasi | 681 | 20 | 701 | 677 | **97** |
| | | Duka la dawa – DLDM (Binadamu) | 2,116 | 149 | 2,265 | 2,096 | **93** |
| | | Duka la dawa – Mifugo | 167 | 24 | 191 | 139 | **73** |
| | | DLDM Mifugo | 396 | 47 | 443 | 365 | **82** |
| | | Zahanati | 153 | 20 | 173 | 153 | **88** |
| | | Vituo vya Afya | 138 | 5 | 143 | 138 | **97** |
| | | Hospitali | 206 | 12 | 218 | 203 | **93** |
| | | **Jumla ndogo** | **4,070** | **281** | **4,351** | **3,961** | **91** |
| 2 | Vipodozi | Vikubwa | 7 | 3 | 10 | 10 | **100** |
| | | Viwanda Kati | 1 | 0 | 1 | 1 | **100** |
| | | Viwanda Vidogo | 16 | 11 | 27 | 14 | **52** |
| | | Maduka ya Jumla | 96 | 10 | 106 | 105 | **99** |
| | | Maduka ya Rejareja | 3,246 | 688 | 3,934 | 3,213 | **82** |
| | | Maghala | 113 | 3 | 116 | 113 | **97** |
| | | Magari ya kubebea vipodozi | 9 | 0 | 9 | 9 | **100** |
| | | **Jumla ndogo** | **3,488** | **715** | **4,203** | **3,465** | **82** |
| 3 | Vifaa tiba | Viwanda vya nje | 20 | 0 | 20 | 8 | **40** |
| | | Viwanda vya ndani | 7 | 0 | 7 | 5 | **71** |
| | | Maduka ya Jumla | 23 | 1 | 24 | 23 | **96** |
| | | Maduka ya Rejareja | 83 | 10 | 93 | 42 | **45** |
| | | **Jumla ndogo** | **133** | **11** | **144** | **78** | **54** |
| | **JUMLA KUU** | | **7,691** | **1,007** | **8,698** | **7,504** | **86** |

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 3, kati ya viwanda na maeneo 8,698 ya biashara za dawa, vipodozi na vifaa tiba yaliyokaguliwa, maeneo 7,504 (86.3%) yamekidhi vigezo. Idadi ya maeneo ya biashara yaliyokaguliwa kwa mwaka huu ni pungufu ya maeneo 579 ikilinganishwa na maeneo 9,277 yaliyokaguliwa mwaka uliopita. Kiwango cha maeneo yaliyokidhi vigezo kimeongeka kwa 4.3% kutoka 82% kwa mwaka 2017/18 mpaka 86.3% kwa mwaka 2018/19.Kuongezeka kwa kiwango cha kukidhi vigezo kwa maeneo yaliyokaguliwa ni kiashiria cha kuonesha kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sheria na uelewa miongoni mwa wadau.

### 2.1.4 Udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi

Mamlaka hudhibiti uingizaji nchini na utoaji nje ya nchi wa bidhaa za dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ili kuhakikisha kuwa zinakidhi vigezo vya usalama na ubora. Bidhaa zinazoruhusiwa kuingia nchini au kusafirishwa nje ya nchi ni zile zilizopewa vibali maalum (import permits) na kusafirishwa nje ya nchi (export permits) baada ya kukidhi vigezo vya usalama na ubora. Mchanganuo wa maombi na vibali vilivyotolewa kwa bidhaa za dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi umeainishwa katika Jedwali Na. 4.




**Jedwali 4: Maombi ya vibali vya kuingiza na kusafirisha bidhaa nje ya nchi**

| Aina ya bidhaa | Maombi yaliyopokelewa | | Vibali vilivyotolewa | | Vibali vilivyokaguliwa | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kuingiza | Kutoa | Kuingiza | Kutoa | Kuingiza | Kutoa |
| Dawa | 4,539 | 127 | 4,491 | 115 | 3,335 | 30 |
| Malighafi za dawa | 582 | - | 578 | - | 358 | - |
| Vipodozi | 1,961 | 1,144 | 1,912 | 1,139 | 1,380 | 357 |
| Malighafi za vipodozi | 1,424 | - | 1,426 | - | 891 | |
| Vitendanishi na vifaa tiba | 5,546 | 360 | 5,508 | 359 | 3,786 | 89 |
| Malighafi za Vitendanishi na vifaa tiba | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **14,053** | **1,631** | **13,916** | **1,613** | **9,751*** | **476*** |



*Idadi ya vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha ni tofauti na vile vilivyotolewa kutokana na muda wa shehena za bidhaa kuingizwa nchini pamoja na ukomo wa kibali kwa miezi sita (6) kabla ya kuisha matumizi
Kwa kuzingatia Jedwali Na.4 hapo juu, kati ya maombi 14,053 ya kuingiza bidhaa nchini, 13,916 (99%) yaliidhinishwa na kati ya maombi 1,631 ya kutoa bidhaa nje ya nchi 1,613 (99%) yaliidhinishwa. Aidha, vibali 10,227 (9,751 vya kuingiza na 476 vya kutoa) vilikaguliwa sawa na 91% ya vibali vyote vilivyotolewa.

### 2.1.5 Ufuatiliaji wa bidhaa za dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi katika soko (PMS)

Sampuli 626 za dawa zilikusanywa ili kuangalia ubora wake ambapo sampuli 418 zilikuwa za dawa zinazofuatiliwa ubora wake kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia (Global Fund) na sampuli 159 zilikuwa ni za dawa mbalimbali kwa mujibu wa Mpango wa TFDA wa ufuatiliaji wa ubora wa dawa.

Mamlaka ilipanga kuchukua sampuli za dawa za binadamu 300 na mifugo 80 kutoka katika mikoa 13 ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Njombe, Dodoma, Morogoro, Manyara, Geita na Shinyanga kwa mujibu wa mpango wa uchukuaji sampuli ulioandaliwa (PMS). Maeneo yaliyohusika kwenye uchukuaji sampuli ni Bohari Kuu ya Dawa (MSD), hospitali za binafsi na serikali, vituo vya afya, zahanati, maduka ya dawa ya jumla na rejereja na Duka la Dawa Muhimu (DLDM).

Jumla ya sampuli 209 za dawa zilikusanywa ambapo kati ya hizo sampuli 159 ni dawa za binadamu na sampuli 50 dawa za mifugo. Dawa za binadamu zilizokusanywa ni dawa za sindano na vidonge aina ya Benzyl Penicillin (44), Benzathine Penicillin (1), Cloxacillin Sodium (7), Artovastatin (61) na Dihydroartemisinin Piperaquine (46). Aidha, sampuli 50 za dawa za mifugo aina ya Albendazole 10% zilikusanywa.

Sampuli zote zilifanyiwa tathmini ya taarifa kwenye vifungashio vya dawa na karatasi za taarifa za dawa (product information review) ambapo yafuatayo yalibainika kwenye baadhi ya sampuli:-

(a) kutowekwa kwa tarehe ya kutengeneza dawa kwenye kifungashio cha awali primary packages na material;
(b) maelekezo ya utunzaji yaliyo kinyume na mwongozo wa lebo kwa ukanda wa IVB;
(c) kutoandikwa kiasi cha kiambata hai ndani ya dawa; na
(d) kutokuwepo kwa jina na anuani ya mtengenezaji kwenye karatasi za taarifa za dawa husika (package insert).

Aidha, sampuli zote za dawa za binadamu na dawa za mifugo zimefanyiwa uchunguzi wa awali na kufaulu vigezo vya ubora. Uchunguzi wa kina wa kimaabara (confirmatory testing) unaendelea kufanyika na utakamilika robo ya kwanza ya mwaka 2019/20.

Chapisho la ufuatiliaji wa ubora wa dawa za kutibu shinikizo la moyo zilizofuatiliwa kwa kipindi cha miaka miwili (2014/15 – 2015/16) liliandaliwa na kuchapishwa mwezi Agosti 2018 katika jarida la kisayansi liitwalo "Pharmaceutical Drug Regulatory Affairs Journal".

Dawa zinazofadhiliwa na Mfuko wa Dunia ni zile za kufubaza makali ya virusi vya Ukimwi, (ARVs) dawa za kutibu ugonjwa wa malaria (Antimaralia) na dawa za kutibu ugonjwa wa Kifua Kikuu.

Kati ya sampuli 418 zilizokusanywa 87 zilikuwa ARVs 215 Antimalaria 116 za kutibu ugonjwa wa kifua kikuu. 383 zilifanyiwa uchunguzi wa kimaabara na zote zilikidhi vigezo na sampuli 35 zinaendelea na majibu yako tayari ya 2019 imeisha kuchunguzwa na matokeo yatakamilika katika robo ya kwanza ya mwaka 2019/20.




#### 1.1.1.1 Ufuatiliaji wa vifaa tiba, vitendanishi na vipodozi

Jumla ya sampuli 246 za vifaa tiba zilikusanywa katika mikoa ya Dar es Salaam, Njombe, Mtwara, Mwanza na Tanga kati ya sampuli 354 zilizopangwa kukusanywa. Uchunguzi wa sampuli 56 kati ya zilizokusanywa umekamilika ambapo sampuli zote zimekidhi vigezo. Aidha tathmini na uchunguzi wa sampuli 190 utakamilika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2019/20.

Vilevile, sampuli 103 za vitendanishi zilikusanywa kati ya sampuli 138 zilizopangwa kukusanywa katika kipindi hicho. Sampuli 59 kati ya zilizokusanywa zilichunguzwa na zote kukidhi vigezo. Uchunguzi wa sampuli zilizobaki utakamilika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2019/20. Mchanganuo wa sampuli zote za vifaa tiba na vitendanishi umeanishwa katika Jedwali Na.5.

**Jedwali 5: Mchanganuo wa sampuli zote za vifaa tiba na vitendanishi zilizokusanywa**

| Bidhaa | Awamu | Idadi ya Sampuli | | | | Maelezo (Kama yapo) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Zilizopangwa kukusanywa | Zilizokusanywa | Zilizochunguzwa | Zilizokidhi vigezo | |
| Vifaa tiba | Ya kwanza | 84 | 56 | 56 | 56 | |
| | Ya pili | 270 | 190 | 190 | Nil | Uchunguzi unaendelea |
| | **Jumla ndogo** | **354** | **246** | **246** | **56** | |
| Vitendanishi | Ya kwanza | 84 | 59 | 59 | 59 | |
| | Ya pili | 54 | 44 | 44 | Nil | Uchunguzi unaendelea |
| | **Jumla ndogo** | **138** | **103** | **103** | **59** | |
| **Jumla kuu** | | **492** | **349** | **349** | **115** | |

Kwa mujibu wa JedwaliNa.5 sampuli zote za vifaa tiba na vitendanishi zilizochunguzwa zilikidhi vigezo vya ubora. Hii inaashiria kwamba bidhaa za vifaa tiba na vitendanishi zilizopo katika soko ni bora kwa watumiaji.

Aidha, sampuli 160 za vipodozi aina ya lipsticks na rangi za kucha zilikusanywa kwa awamu ya pili kwenye

mikoa ya Arusha na Dar es Salaam baada ya Mamlaka kupokea malalamiko ya madhara toka kwa watumiaji wa bidhaa hizi. Matokeo ya uchunguzi yatatolewa ndani ya kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2019/20.
2.1.6 2.1.7 Ufuatiliaji wa usalama na matukio yanayohusiana na dawa na vifaa tiba



### 1.1.1.1 Ufuatiliaji wa usalama wa dawa

Taarifa 1,320 za madhara yanayohisiwa kusababishwa na matumizi ya dawa na chanjo zilipokelewa na kufanyiwa tathmini. Taarifa zote ziliingizwa kwenye kanzidata ya Vigiflow inayotumiwa na wanachama wa Mpango wa Kimataifa wa Ufuataliaji wa Usalama wa Dawa unaoratibiwa na Shirika la Afya Duniani kupita kituo cha Uppsala Monitoring Centre nchini Sweden. Kati ya taarifa 1,320 zilizowekwa kwenye Vigiflow, taarifa mbili (2) zilihusiana na chanjo ya Pertusis na Tetanus. Vile vile taarifa 369 zilipokelewa kwa njia ya simu kupitia mfumo wa USSD na kufanyiwa tathmini. Taarifa zote zilijadiliwa kwenye kikao cha Kamati ya Usalama wa Dawa kilichofanyika tarehe 27 Juni 2019 na hapakuwa na madhara mapya na hatarishi yaliyohitaji kuchukuliwa hatua zaidi.
Kwa mara ya kwanza kumekuwa na ongezeko la kasi ya utoaji wa taarifa za madhara ya dawa kwa zaidi ya asilimia 400 ilinganishwa na tarifa zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2017/2018. Sababu ya ongezeko la taarifa hizo ni pamoja na ushirikishwaji wa wafamasia walio katika mafunzo (intern pharmacists) waliopo katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili.
Vile vile, uhamasishaji wa utoaji wa taarifa za madhara ya dawa ulifanyika kwa watumishi wa afya wapatao 296 katika mikoa ya Dar es salaam (28), Iringa (96), Njombe (44), na Tanga (128). Kazi hiyo ilifanyika sambamba na ukaguzi wa vyumba vilivyotengwa kwa ajili ya kazi ya kuratibu kazi za usalama wa dawa ngazi ya mkoa katika mikoa tajwa.

### 1.1.1.2 Ufuatiliaji wa usalama na matukio yanayohusiana na vifaa tiba na vitendanishi

Taarifa 26 za matukio ya vifaa tiba zilipokelewa na taarifa 24 kati ya hizo sawa na 92% zilifanyiwa tathmini. Tathmini na ufuatiliaji wa vifaa tiba viwili (2) vilivyobaki imepangwa kufanyika mwaka wa fedha 2019/20.
Aidha, uhamasishaji juu ya utoaji wa taarifa za madhara ya vifaa tiba na vitendanishi ulifanyika kwa watoa huduma za afya 504 katika mikoa ya Songwe, Rukwa, Kigoma na Mara
1.1.1.3 Utekelezaji wa Miradi ya PAVIA, PROFORMA na SMERT

Miradi ya PROFORMA, PAVIA na SMERT inafadhiliwa na EDCTP kwa lengo la kusaidia kujenga uwezo na kuimarisha mifumo katika maeneo ya ufuatialiji wa usalama na ubora wa dawa pamoja na udhibiti wa majaribio ya dawa. Miradi hii ilianza kutekelezwa mwezi Aprili, 2018 ambapo mradi wa PROFOMA ni wa muda wa miaka mitano (5), mradi wa PAVIA ni wa muda wa miaka minne (4) na mradi wa SMERT ni wa muda wa miaka miwili (2).

**(a) Mradi wa PROFORMA**
Kazi zifutazo za mradi wa PROFORMA zilifanyika;

i. Kuandaa andiko la ufuatiliaji wa karibu wa usalama wa dawa ya Ivermectin na Albendazole na kuwasilisha andiko hilo kwenye Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ili kuomba kibali;
ii. Kuandaa Mpango wa utekelezaji wa kazi mbalimbali zilizopangwa kufanyika kupitia mradi huo;
iii. Kufanya tathmini ya mifumo ya Pharmacovigilance mwanzoni mwa mradi ili kuweza kupima ipasavyo matokeo na mafaniko ya mradi mwishoni mwa utekelezaji wake;
iv. Kuandaa fomu na vitendea kazi vingine vya ufuatiliaji wa karibu wa dawa za Ivermectin na Albendazole;
v. Kuandaa andiko la ufuatiliaji wa usalama wa chanjo ya Saratani ya Shingo la kizazi (HPV Vaccine);
vi. Kufanya mkutano na wadau wa ndani wa mradi wa PROFORMA;
vii. Kazi ya ufuatiliaji wa ubora na usalama wa dawa za Ivermectin na Albendazole ilifanyika katika Mkoa wa Tanga ambapo watu 184 waliopewa dawa za Ivermectin na Albendazole walifuatiliwa. Kati ya watu hao, 164 walionekana kuwa na vinasaba vya ugonjwa wa matende na mabusha. Pia watu wawili (2) walionekana kuwa na vimelea vya ugonjwa wa matende na mabusha; na
viii. Mkutano wa mwaka wa PROFORMA ulifanyika nchini Rwanda ambapo washiriki watatu walihudhuria na kupata mafunzo ya wiki moja.

**(b) PAVIA**

Kwa upande wa mradi wa PAVIA, kazi zifuatazo zilitekelezwa;

i. Tathmini ya hali ya mifumo iliyopo kabla ya utekelezaji wa mradi wa PAVIA;
ii. Mkutano wa ndani wa wadau;
iii. Mpango Kazi wa mradi uliandaliwa; na
iv. Ofisi mpya za kuratibu masuala ya Pharmacovigilance katika ngazi ya mikoa zilifuatiliwa na kupatikana. Aidha, kompyuta 20 na printa 20 kwa ajili ya ofisi tajwa zilinunuliwa na kupelekwa kwa wahusika kwa ajili ya kazi ya ufuatiliaji wa usalama wa dawa.

Vile vile, Mkutano wa mwaka wa nchi zote zinazoshiriki katika mradi wa PAVIA ulifanyika nchini Ethiopia tarehe 1-6 April 2019. Mafunzo ya ufuatiliaji wa usalama wa dawa kwa nchi shiriki kwenye mradi huu yalifanyika tarehe 8 -13 Aprili 2019.

(c) SMERT:

Kazi ya kuainisha maeneo ya Majaribio ya dawa ambayo yanatakiwa kuwianishwa chini ya nchi za Afrika Mashariki ilifanyika ikiwa ni pamoja na kuhudhuria kikao nchini Afrika Kusini cha kujadili maeneo tajwa tarehe 20 - 23 Mei, 2019. Mkutano wa wadau wa mradi wa SMERT kujadili maeneo tajwa utafanyika mwezi Julai, 2019. Vile vile mafunzo maalum ya udhibiti wa majaribio ya dawa yalifanyika kwa watoa huduma za afya, watafiti na wanafunzi wa Shahada ya Uzamili wapatao 20 kutoka katika Chuo Kikuu cha KCMC.

2.1.8 Mpango wa Uwianisho wa Taratibu za Udhibiti wa Dawa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

2.1.7.1 Tathmini ya kikanda ya maombi ya usajili wa dawa

Maombi 46 ya usajili wa dawa za binadamu yalipokelewa katika mchanganuo ufuatao; 23 mapya na 23 ya hoja. Hapakuwa na baki ya maombi mapya. Jumla ya maombi 36 yalifanyiwa tathmini ya pamoja ambapo 16 ni mapya na 20 majibu ya hoja kama ilivyoainishwa kwenye jedwali Na. 6.

Maombi 18 yalipendekezwa kupewa usajili na tayari nchi wanachama wametaarifiwa kuhusu mapendekezo haya na hivyo kuendelea na taratibu za usajili pale waombaji watakapokamilisha taratibu za nchi husika. Aidha Mamlaka imeidhinisha usajili wa dawa 15 na taratibu za usajili wa dawa tatu (3) unaendelea.

**Jedwali Na. 6: Tathmini na usajili wa dawa za binadamu kikanda**

| Aina ya Usajili | Aina | Baki ya Juni 30, 2018 | Pokelewa | Jumla ndogo | Tathminiwa | Baki, Juni, 2019 | Sajiliwa | Pendekezwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kikanda | Mapya | 0 | 23 | **23** | 16 | 7 | 0 | 0 |
| | Hoja | 0 | 23 | **23** | 20 | 3 | 15 | 3 |
| **Jumla** | | **0** | **46** | **46** | **36** | **10** | **15** | **3** |

**2.1.7.2 Utekelezaji wa mfumo wa kieletroniki (IMIS) awamu ya pili**

Mamlaka iliboresha mfumo wa kielektroniki (IMIS) ili kuwezesha upokeaji wa maombi ya usajili wa bidhaa kwa

njia ya mtandao (online) ili kurahisisha na kuharakisha utoaji huduma kwa wateja. Mfumo upo katika hatua ya majaribio amabapo watumishi na baadhi ya wateja wameshiriki kuutumia na kutoa maoni yao kwa ajili ya kuendelea kuboresha. Aidha, jumla ya Server nne zenye uwezo wa kubeba na kutunza taarifa za maombi ya usajili wa bidhaa zimesimikwa katika jengo la TFDA Ofisi ndogo ya Dar es Salaam.

### 2.1.9 Ukaguzi maalum wa dawa za binadamu na mifugo

Ukaguzi maalum wa dawa za binadamu na mifugo ulifanyika katika mikoa ya Arusha na Kigoma ambapo maeneo 162 yalikaguliwa yakiwemo maduka ya dawa za binadamu 12, maduka ya dawa muhimu za binadamu 68 na maduka ya dawa za mifugo 80 kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 7 hapa chini.

**Jedwali Na. 7: Mchanganuo wa maeneo yaliyokaguliwa**

| Na. | Aina ya Jengo | Mkoa | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Kigoma | Arusha | |
| 1. | Maduka ya Dawa za Binadamu | 9 | 3 | 12 |
| 2. | Maduka ya Dawa za Mifugo | 13 | 67 | 80 |
| 3. | DLDM (Binadamu) | 19 | 49 | 68 |
| 4. | Stoo ya dawa za binadamu ya Wilaya | 0 | 1 | 1 |
| 5. | Nyumba za Makazi | 1 | 0 | 1 |
| | **Jumla** | **42** | **120** | **162** |

**Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-**

**Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-**



(a) dawa nyingi zilizopo kwenye soko zimesajiliwa na Mamlaka;
(b) dawa za mifugo ambazo hazijasaliwa zenye thamani ya takriban TZS 25,021,300 zilikamatwa;
(c) dawa za binadamu ambazo haziruhusiwi kuuzwa kwenye maduka ya dawa muhimu zenye thamani ya takriban TZS 19,449,382 zilikamatwa;
(d) dawa bandia ya mifugo aina ya trypamidium samorin inayosadikiwa kutengenezwa na kiwanda cha Merial Ufaransa ilikamatwa kwenye duka moja;
(e) dawa za kutibu ugonjwa wa malaria, dawa za kutibu kifua kikuu na vifaa tiba vya serikali vilikamatwa kwenye maduka ya watu binafsi.

Hatua zilizochukuliwa kutokana na ukaguzi huo ni pamoja na kuteketeza bidhaa zisizofaa baada ya wahusika kukubali kulipa gharama za uteketezaji na wale waliokutwa na dawa za serikali walifunguliwa majalada ya kesi polisi.

### 2.1.10 Ukaguzi maalum wa OPSON VIII

Ukaguzi maalum uliopewa jina la Operesheni OPSON VIII ulifanyika kwa kushirikiana na taasisi za Serikali katika mikoa ya Dar es salaam, Mbeya, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mwanza, Arusha na Geita. Majengo 322 yalikaguliwa kama yalivyooneshwa katika jedwali Na. 8

**Jedwali Na. 8: Mchanganuo wa maeneo yaliyokaguliwa wakati wa Operesheni OPSON VIII**

| Na. | Mkoa | Maduka ya Vipodozi | Eneo la Makazi | Maduka ya Chakula | Zahanati | Maghala ya Chakula | Maduka ya Dawa | DLDM | Ujenzi Vifaa | Hospitali | Tiba asili | Vifaa vya magari | Viatu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kigoma | 6 | 0 | 8 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **19** |
| 2. | Mwanza | 9 | 1 | 17 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | **34** |
| 3. | Kilimanjaro | 7 | 0 | 5 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **18** |
| 4. | Geita | 2 | 0 | 5 | 0 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **13** |
| 5. | Arusha | 5 | 0 | 12 | 0 | 0 | 10 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 | 0 | **40** |
| 6. | Dodoma | 10 | 0 | 8 | 0 | 0 | 9 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **29** |
| 7. | Dar es Salaam | 29 | 0 | 63 | 0 | 0 | 32 | 0 | 0 | 3 | 0 | 2 | 2 | **131** |
| 8. | Mbeya | 15 | 0 | 15 | 0 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **38** |
| | **Jumla** | **83** | **1** | **133** | **1** | **5** | **70** | **6** | **13** | **5** | **1** | **2** | **2** | **322** |

**Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-**

(a) vipodozi vilivyopigwa marufuku vyenye thamani ya takriban TZS 122,460,015 vilikamatwa;
(b) bidhaa za chakula zenye thamani ya takriban TZS 4,397,000 zilikamatwa kutokana na kutokidhi matakwa ya Sheria;
(c) Asilimia 28 ya maduka ya dawa yaliyokaguliwa yalikutwa yakikihifadhi dawa katika jotoridi lisilostahili; na
(d) baadhi ya maduka ya dawa yalikutwa yakiwa na dawa za Serikali.

Kutokana na ukaguzi huo hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa kwa wahusika ikiwemo kufungua majalada matatu (3) ya kesi katika vituo vya polisi katika mikoa ya Dodoma, Kigoma na Mwanza ambapo uchunguzi bado unaendelea.



### 2.1.11 Ukaguzi maalum wa dawa za tiba zenye asili ya kulevya

Ukaguzi huu ulifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya ambapo majengo 124 yalikaguliwa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na.8: Maeneo ya utoaji wa dawa za tiba zenye asili ya kulevya yalikaguliwa**

| Na. | Mkoa | Viwanda | Hospitali | Vituo vya Afya | Bohari ya Dawa (MSD) | Maduka ya dawa za binadamu | Maduka ya Dawa Muhimu za Binadamu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | 2 | 10 | 0 | 2 | 22 | 4 | **40** |
| 2. | Dodoma | 0 | 05 | 0 | 01 | 24 | 01 | **31** |
| 3. | Mwanza | 0 | 8 | 1 | 01 | 2 | 0 | **12** |
| 4. | Arusha | 0 | 7 | 0 | 0 | 13 | 3 | **23** |
| 5. | Mbeya | 0 | 6 | 1 | 1 | 7 | 3 | **18** |
| | **JUMLA** | **2** | **36** | **2** | **5** | **68** | **11** | **124** |

Matokeo ya operesheni hiyo yalibaini kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha kwa upande wa dawa za tiba zenye asili ya kulevya na hivyo Mamlaka itaimarisha udhibiti zaidi katika eneo hilo.



## 2.2 KUHAKIKISHA USALAMA NA UBORA WA CHAKULA

Mamlaka ina jukumu la kudhibiti usalama na ubora wa vyakula vinavyozalishwa, kuingizwa, kusambazwa na kuuzwa nchini kwa matumizi ya binadamu ili kulinda afya ya jamii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mamlaka ilitekeleza kazi mbalimbali kwa mwaka 2018/19 ili kutimiza lengo hili kama ilivyoainishwa katika vipengele 2.2.1- 2.2.13.

### 2.2.1 Usajili wa bidhaa za chakula

Kabla ya kusajiliwa, bidhaa za chakula hufanyiwa tathmini ya taarifa za kisayansi za usalama na ubora ikijumuisha taarifa za viambato na vikolezo vilivyotumika katika utengenezaji wake, vifungashio, taarifa za lebo na mifumo ya uzalishaji kwa kuzingatia kanuni, miongozo na viwango vya kitaifa na kimataifa.

Jumla ya maombi 3,286 ya usajili wa bidhaa za chakula yalipokelewa ambapo maombi 2,799 yalikuwa mapya na 487 yalikuwa ya kuhuisha usajili. Aidha, Mamlaka ilikuwa na jumla ya maombi 67 yaliyobaki bila kufanyiwa tathmini kwa kipindi cha mwaka 2017/18 hivyo kufanya idadi ya maombi yaliyohitaji kufanyiwa tathmini kuwa 3,353. Jumla ya maombi 3,353 sawa na 100% ya maombi yote yalifanyiwa tathmini ambapo 2,876 sawa na 86% yalikidhi vigezo na hivyo kusajiliwa. Maombi 140 yalikataliwa usajili na 337 yalikuwa na hoja kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 9.

Jedwali Na. 9: Idadi ya maombi ya usajili wa bidhaa za chakula.

| Maelezo | Baki kutoka Juni, 2018 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Hoja | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mapya | 62 | 2,799 | 2,861 | 2,861 | 2,432 | 124 | 305 | 0 |
| Kuhuishwa | 5 | 487 | 492 | 492 | 444 | 16 | 32 | 0 |
| **Jumla** | **67** | **3,286** | **3,353** | **3,353** | **2,876** | **140** | **337** | **0** |

### 2.2.2 Tathmini ya matangazo ya biashara, lebo na mabadiliko ya bidhaa zilizosajiliwa

Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 153 yanayohusu tathmini ya matangazo ya biashara za chakula, lebo na mabadiliko ya bidhaa zilizosajiliwa ambapo maombi yote yalitathminiwa na 116 kati yake yaliidhinishwa na 37 yalikuwa na hoja kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10 : Maombi mengine yanayohusu usajili wa bidhaa za chakula**

| Na. | Maelezo | Baki 2017/18 | Pokelewa 2018/19 | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Hoja | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matangazo | 0 | 29 | **29** | 29 | 23 | 0 | 6 | 0 |
| 2 | Lebo | 0 | 94 | **94** | 94 | 66 | 0 | 28 | 0 |
| 3 | Mabadiliko | 0 | 30 | **30** | 30 | 27 | 0 | 3 | 0 |
| **Jumla** | | **0** | **153** | **153** | **153** | **116** | **0** | **37** | **0** |

### 2.2.3 Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya chakula

Maeneo ya biashara za bidhaa za chakula husajiliwa kwa lengo la kutambua majengo ambako bidhaa hizo huzalishwa, kuhifadhiwa, kusambazwa na kuuzwa. Mfumo huu husaidia kuhakikisha kuwa maeneo husika yanakidhi vigezo ili kutoathiri usalama na ubora wa chakula. Mchanganuo wa vibali vya biashara vilivyotolewa na maeneo yaliyosajiliwa katika kipindi hiki umeainishwa katika Majedwali Na. 11 (a) na (b).

**Jedwali Na. 11(a): Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya chakula**

| Na. | Aina ya jengo | | Baki kutoka mwaka 2017/18 | Yaliyopokelewa | | Jumla | Yaliyofanyiwa kazi | Yaliyosajiliwa | Hoja | % Yaliyokidhi vigezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mapya | Huisha | | | | | |
| 1 | Viwanda | Vikubwa | 2 | 28 | 108 | **138** | 133 | 132 | 1 | 99.2% |
| | | Kati | 1 | 76 | 303 | **380** | 375 | 353 | 22 | 94.1% |
| | | Vidogo | 20 | 344 | 387 | **751** | 741 | 620 | 121 | 83.7% |
| | Maghala | | 20 | 282 | 324 | **626** | 614 | 527 | 87 | 85.8% |
| | Hoteli | | 20 | 141 | 398 | **559** | 561 | 466 | 95 | 83.1% |
| | Maduka jumla na rejareja | | 32 | 1173 | 1642 | **2847** | 2848 | 2835 | 13 | 99.5% |
| | *Super markets* | | 0 | 74 | 190 | **264** | 262 | 233 | 29 | 88.9% |
| | Machinjio | | 0 | 3 | 5 | **8** | 8 | 8 | 0 | 100.0% |
| | Magari ya kubebea chakula | | 0 | 419 | 342 | **761** | 761 | 759 | 2 | 99.7% |
| | Mabucha | | 0 | 10 | 12 | **22** | 22 | 22 | 0 | 100.0% |
| | **Jumla** | | **95** | **2,550** | **3,711** | **6,356** | **6,325** | **5,955** | **370** | **94.2%** |

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 11(a) hapo juu, kati ya maombi 6,356 ya usajili wa maeneo ya biashara yaliyopokelewa, maombi 6,325 (99.5%) yalifanyiwa kazi ambapo majengo 5,955 (93%) yalisajiliwa kwa kuwa yalikidhi vigezo.

**edwali Na. 11(b): Mchanganuo wa makundi ya viwanda vya chakula vilivyosajiliwa kwa kipindi cha Julai, 2018 – Juni, 2019 kwa kila kanda**

| Na. | Ofisi ya Kanda | Viwanda vidogo (Small scale food) | Viwanda vya kati (Medium scale) | Viwanda vikubwa (Large scale) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mashariki | 109 | 14 | 11 | **134** |
| 2 | Kaskazini | 35 | 7 | 2 | **44** |
| 3 | Ziwa (Mashariki na Magharibi) | 48 | 13 | 9 | **70** |
| 4 | Kusini | 39 | 4 | 2 | **45** |
| 5 | Magharibi | 15 | 5 | 0 | **20** |
| 6 | Nyanda za Juu Kusini | 46 | 26 | 3 | **75** |
| 7 | Kati | 52 | 7 | 1 | **60** |
| | **Jumla** | **344** | **76** | **28** | **448** |

### 2.2.4 Ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara za chakula

Maeneo yanayojihusisha na biashara ya chakula ikiwemo viwanda vya uzalishaji na majengo ya kuuzia hususan maghala, maduka ya chakula, migahawa, mahoteli, machinjio na magari ya kubeba vyakula hukaguliwa kila

mara ili kuhakiki mifumo ya utengenezaji na mazingira ya uzalishaji, usambazaji, uhifadhi na uuzaji na hivyo kuimarisha udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa za chakula. Jedwali Na. 12 limeainisha mchanganuo wa maeneo yaliyokaguliwa katika mwaka huu.

**Jedwali Na. 12: Ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara ya chakula**

| | Aina ya Biashara | Maeneo yaliyokaguliwa | | | Yaliyokidhi Vigezo | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyosajiliwa | Yasiyosajiliwa | Jumla | Idadi | % |
| 1 | Viwanda Vikubwa | 146 | 33 | 179 | 131 | 73 |
| | Viwanda Kati | 402 | 62 | 464 | 394 | 85 |
| | Viwanda Vidogo | 815 | 603 | 1418 | 900 | 63 |
| | **Jumla ndogo** | **1,363** | **698** | **2,061** | **1,425** | **69** |
| 2 | Maghala | 478 | 131 | 609 | 532 | 87 |
| | Hoteli | 358 | 102 | 460 | 276 | 60 |
| | Migahawa | 10 | 30 | 40 | 11 | 28 |
| | Maduka Jumla | 1,884 | 771 | 2,655 | 1,987 | 75 |
| | Maduka Rejareja | 2,458 | 783 | 3,241 | 2,963 | 91 |
| | *Super market* | 399 | 41 | 440 | 334 | 76 |
| | Machinjio | 37 | 134 | 171 | 45 | 26 |
| | Bucha | 156 | 63 | 219 | 107 | 49 |
| | Magari ya kubeba chakula | 155 | 4 | 159 | 138 | 87 |
| | **Jumla ndogo** | **5,935** | **2,059** | **7,994** | **6,393** | **80** |
| **Jumla** | | **7,298** | **2,757** | **10,055** | **7,818** | **78** |

Kwa kuzingatia Jedwali Na. 12 hapo juu, kati ya maeneo 10,055 yaliyokaguliwa, maeneo 7,818 (78%) yalikidhi vigezo. Idadi ya maeneo yaliyokidhi vigezo ni ongezeko la maeneo 725 sawa na 10% ikilinganishwa na maeneo 7,093 yaliyokidhi vigezo mwaka 2017/18. Hata hivyo suala la udhibiti wa machinjio bado lina changamoto nyingi kwa kuwa mengi yanamilikiwa na halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji. Aidha, wamiliki wa maeneo ambayo hayakukidhi vigezo vya usalama na matakwa ya sheria walipewa maelekezo ya kurekebisha kasoro zilizobainishwa.

Vile vile, jumla ya viwanda 10 vya kuzalisha vyakula kwa ajili ya mahitaji maalum ya lishe (High risk foods for special nutritional purposes) vilivyoko nje ya nchi vilikaguliwa. Viwanda hivyo ni vya kuzalisha maziwa mbadala ya watoto nchini Poland (1), vyakula vya kulikiza nchini Kenya (1) na viwanda vya kuzalisha vyakula nyongeza (food supplements) vilivyopo India (2), Italia (2), China (2), Ubelgiji (1) na Malaysia (1). Baadhi ya kasoro zilizobainika katika ukaguzi huo ni pamoja na kutozingatiwa kwa kanuni bora za uzalishaji wa chakula ambapo wahusika walielekezwa kufanya marekebisho.

### 2.2.5 Ukaguzi wa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoongezwa virutubishi

TFDA husimamia utekelezaji wa Kanuni za uongezaji virutubishi kwenye vyakula ili kuwezesha kufikia lengo la kuboresha hali ya lishe nchini bila kusababisha madhara ya kiafya. Aina ya vyakula vinavyoongezwa virutubishi kwa mujibu wa Kanuni na aina ya virutubishi vinavyoongezwa ni chumvi (madini joto), unga wa ngano na unga wa mahindi (madini chuma, zinki, vitamin $B_{12}$ na folate) na mafuta ya kula (vitamin A).

Jumla ya viwanda 67 vinavyozalisha na kuongeza virutubishi kwenye vyakula vilikaguliwa ambapo vitano (5) ni vya mafuta ya kula, 50 vya unga wa mahindi, vitatu (3) vya chumvi, viwanda vitano (5) vya unga wa ngano na

mashamba manne (4) ya kuzalisha chumvi. Jumla ya viwanda 56 sawa na 84% ya vilivyokaguliwa vilikuwa vinaongeza virutubisho kwenye bidhaa husika. Mamlaka itaendelea kufanya ufuatiliaji na kutoa mafunzo wasindikaji ili kuimarisha mkakati wa utubishaji wa vyakula.

### 2.2.6 Ufuatiliaji wa bidhaa za chakula katika soko (post-marketing surveillance)

Mamlaka ilifanya ufuatiliaji na uchunguzi wa sukari na bidhaa zinazotengenezwa kwa kutumia sukari ili kujiridhisha kuhusu usalama wake. Hatua hii ilichukuliwa kufuatia madai ya uwepo wa sukari iliyochafuliwa na madini tembo (heavy metals) katika mojawapo ya nchi jirani. Jumla ya sampuli 255 zilichukuliwa kutoka maeneo mbalimbali katika soko na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara ambapo matokeo yalionesha kuwa bidhaa hizo hazikuwa na uchafuzi wa madini tembo. Pamoja na matokeo hayo, TFDA itaendelea kuimarisha udhibiti wa usalama na ubora wa sukari pamoja na bidhaa zinazozalishwa na sukari ili kuendelea kulinda afya ya jamii.

Vile vile, Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ilifanya ufuatiliaji wa vinywaji vya kuongeza nguvu mwilini (energy drinks) pamoja na matumizi sahihi ya rangi katika usindikaji wa chakula. Kupitia ufuatiliaji huo, jumla ya maeneo 72 yalikaguliwa katika mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya ambapo takriban kilogramu 21.6 za rangi ya chakula (food colour) aina ya tartrazine zilikamatwa katika maeneo ya usindikaji na kuondolewa kutokana na ukiukwaji wa kanuni za matumizi sahihi ya rangi kwenye vyakula. Aidha, ukaguzi haukubaini uwepo wa vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks) visivyokidhi matakwa ya kisheria. Kufuatia matokeo hayo, mamlaka itaendelea kuimarisha udhibiti ili kuhakikisha matumizi sahihi ya rangi katika usindikaji wa vyakula.

Kwa lengo la kubaini hali ya uchafuzi wa sumukuvu na mabaki ya dawa za mifugo katika maziwa ya ng'ombe yasiyosindikwa (cow's raw milk), mamlaka ilichukua jumla ya sampuli 300 za maziwa ya ngombe katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ambapo uchunguzi huo bado unaendelea.

### 2.2.7 Mafunzo kwa wasindikaji wadogo wa vyakula

Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Viwango nchini (TBS), Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo nchini (SIDO) na Halmashauri za Wilaya ilifanya mafunzo yanayohusu usalama wa chakula kwa wasindikaji wadogo wa vyakula ambapo jumla ya wasindikaji 530 walishiriki kutoka Mikoa ya Njombe (106), Shinyanga (84), Kagera (112), Morogoro (135) na Mara (93). Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha wasindikaji ili waweze kukidhi matakwa ya kuzalisha chakula salama.

### 2.2.8 Mikutano ya wadau wa usalama wa chakula

Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ilifanya mkutano wa wadau uliongozwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na kujadili mchango wa taasisi za serikali na changamoto katika kuwezesha viwanda vya chakula nchini. Mkutano huo ulihudhuriwa na taasisi zenye mchango katika uwekezaji wa viwanda vya chakula ambazo ni TIC, TBS, NDC na TIRDO ambapo jumla ya wadau 147 walishiriki.

Vile vile, mamlaka kwa kushirikiana na Jumuiya ya Umoja wa Afrika iliratibu maadhimisho ya siku ya uhakika wa chakula na lishe barani Afrika. Kupitia maadhimisho hayo, washiriki walipata fursa ya kujadili na kuweka mikakati ya kuhakikisha usalama wa chakula ili kuboresha hali ya uhakika wa chakula na lishe.

Aidha, mamlaka ilifanya mkutano wa wadau wa chakula kwa lengo la kuwahamasisha juu ya taratibu na matakwa ya sheria katika usajili wa bidhaa ili kuwawezesha kusajili bidhaa zao. Jumla ya wadau 245 katika mikoani ya Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Mwanza, Shinyanga na Kagera walishiriki.

### 2.2.9 Kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya usalama wa chakula

Mamlaka ilifanya mikutano wa watoa huduma ya chakula katika mikusanyiko ya watu wengi (mass food caterers) kama vile harusi, misiba na mikutano katika mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Katavi na Tabora. Lengo la mikutano hiyo ni kuimarisha udhibiti wa sekta hiyo ili kuhakilisha kuwa huduma hiyo inatolewa bila kuathiri usalama wa chakula na kusababisha madhara ya kiafya kwa walaji. Jumla ya watoa huduma 431 walishiriki na kupata fursa ya kujadili kuhusu matakwa ya sheria na kuweka mikakati ya kuboresha mazingira ya utoaji huduma ya chakula kwenye mikusanyiko ili kuhakikisha usalama wa chakula kinachoandaliwa.

Mamlaka ilitoa semina kwa wanahabari kuhusu masula mbalimbali ya usalama wa chakula kwa lengo la kuwapa uelewa ili waweze kuelimisha jamii kuepuka na pia kukabiliana na madhara yatokanayo na chakula kisicho salama. Kupitia mafunzo hayo, jumla ya wanabari 55 kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini walishiriki. Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa maadhimisho ya siku ya Usalama wa Chakula Duniani kwa lengo la kuhakilisha kuwa kila mdau anatambua wajibu wake katika kuhakikisha usalama wa chakula.

Kufuatia mkutano huo, taasisi zilizoshiriki zilielekezwa kuendelea kuwawezesha wadau wanaoonesha nia ya kuanzisha viwanda vya chakula pamoja na walio na viwanda ili kufanikisha uwekezaji katika sekta hiyo hapa nchini.
Aidha, kwa lengo la kukabiliana na magonjwa yatokanayo na chakula kisicho salama, mamlaka ilitoa elimu kwa jamii ya wafugaji katika wilaya ya Ngorongoro kuhusiana na athari za ulaji wa nyama isiyo salama kama vile nyama ya mizoga au mifugo yenye ugonjwa ili kuepuka madhara ya kiafya.

**2.2.10 Utekelezaji Mikakati ya Udhibiti wa Sumukuvu**

Mamlaka ilifanya mkutano wa Kamati endeshaji ya kitaifa ya udhibiti wa Sumukuvu (National Steering Committee on Mycotoxins Control) ili kujadili na kutoa mapendekezo ya kufanikisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kudhibiti uchafuzi wa sumukuvu katika chakula.

Kwa lengo la kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa sumukuvu katika nafaka, karanga na mazao yake, mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Taasisi ya Chakula na Lishe na wataalam wa afya, kilimo na mifugo katika Halmashauri ilitoa elimu kwa wasindikaji wa unga wa nafaka na siagi ya karanga (peanut butter) juu ya sumukuvu na udhibiti wake. Jumla ya wadau 152 katika mikoa ya Arusha, Dodoma na Morogoro walipata mafunzo hayo.

Aidha, Mamlaka iliandaa mwongozo wa mafunzo kuhusiana na sumukuvu na mikakati ya udhibiti wake ambao utatumika katika kutoa mafunzo kwa wadau ili kuimarisha udhibiti wa sumukuvu katika chakula. Vilevile, vipeperushi na mabango kwa ajili ya uelimishaji jamii kuhusu sumukuvu viliandaliwa na kuchapishwa.

**2.2.11 Utekelezaji wa mkakati wa ufuatiliaji wa magonjwa yatokanayo na chakula**

Mamlaka ilitoa mafunzo kwa jumla ya wataalam wa afya 138 wa fani za fundi sanifu maabara, afisa afya na afisa tabibu kutoka halmashauri zote za mikoa ya Kagera, Simiyu, Geita, Shinyanga na Iringa ili kuimarisha uwezo katika kufanya ufuatiliaji wa magonjwa yatokanayo na chakula, kuyatolewa taarifa na kukabiliana nayo.

Hali kadhalika, mamlaka iliwezeshwa kutumia mfumo wa Taifa wa utoaji wa taarifa za magonjwa yanayotokea sehemu zote nchini. Hatua hii itaboresha uwezo wa mamlaka katika kupata taarifa za magonjwa yatokanayo na chakula nchini kwa urahisi na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo.

**2.2.12 Udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji wa chakula nje ya nchi**

Udhibiti wa uingizaji wa bidhaa za chakula nchini na usafirishaji nje ya nchi hufanyika ili kuhakikisha kuwa bidhaa zote za vyakula na malighafi zinazotumika kutengeneza vyakula zinakidhi vigezo vya usalama na ubora. Jumla ya vibali 8,533 vya kuingiza vyakula nchini na vibali 1,757 vya kusafirisha vyakula nje ya nchi vilitolewa kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 13.




**Jedwali Na. 13: Maombi ya vibali vya kuingiza nchini na kusafirisha chakula nje ya nchi**

| Aina ya bidhaa | Maombi yaliyopokelewa | | Vibali vilivyotolewa | | Vibali vilivyokaguliwa | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kuingiza | Kutoa | Kuingiza | Kutoa | Kuingiza | Kutoa |
| Chakula | 6,601 | 2,524 | 6,533 | 2,502 | 6,497 | 1,966 |
| Malighafi za chakula | 1932 | 0 | 1914 | 0 | 1902 | 0 |
| **Jumla** | **8,533** | **2,524** | **8,447** | **2,502** | **8,399** | **1,966** |

Kwa kuzingatia Jedwali Na.13 hapo juu, kati ya maombi 8,533 ya kuingiza nchini bidhaa za chakula, 8,447 (99%) yaliidhinishwa na kati ya maombi 2,524 ya kusafirisha nje ya nchi bidhaa za chakula, 2,502 (99%) yaliidhinishwa. Aidha, vibali 10,365 (8,399 vya kuingiza vyakula nchini na 1,969 vya kutoa vyakula nje ya nchi) vilikaguliwa ambavyo ni sawa na 95% ya vibali vyote vilivyotolewa.

### 2.2.13 Uteketezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na usalama

Mamlaka imeteketeza bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ambazo hazikidhi vigezo vya ubora na usalama na ufanisi ili kuepusha bidhaa husika zisitumiwe na walaji. Bidhaa zilizoteketezwa zinajumuisha zilizoombewa kibali (voluntary disposal) na wateja wenyewe kutokana na kuisha muda wa matumizi na bidhaa zilizokamatwa katika kaguzi mbalimbali kwa kutokusajiliwa, kuwa duni/bandia baada ya kubainika kutokidhi vigezo vya uchunguzi wa kimaabara. Uzito na thamani za bidhaa zilizoteketezwa kwa mwaka huu imeainishwa katika Jedwali Na. 14.

**Jedwali Na.14: Mchanganuo wa bidhaa zilizoteketezwa kati ya Julai, 2018 – Juni, 2019**

| Na. | Aina ya bidhaa | Mchanganuo | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Vilivyotolewa taarifa | | Vilivyokamatwa | |
| | | Uzito (Tani) | Thamani (TZS) | Uzito (Tani) | Thamani (TZS) |
| 1 | Chakula | 1839.36 | 2,412,426,099 | 132,837.07 | 585,356,772 |
| 2 | Dawa za Binadamu | 1068.4 | 7,078,257,419 | 4,930.30 | 405,913,280 |
| 3 | Dawa za Mifugo | 0 | 0 | 0.77 | 48,855,500 |
| 4 | Vipodozi | 15 | 98,902,339 | 14.329 | 225,257,335 |
| 5 | Vifaa tiba | 0 | 0 | 0.021 | 15,110,000 |
| **Jumla** | | **2,922.76** | **9,589,585,857** | **137,782.49** | **1,280,492,887** |

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 14 hapo juu, jumla ya tani 137,782.49 za bidhaa zenye thamani ya takriban TZS 1,280,492,887.00 ziliteketezwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 14 hapo juu, jumla ya tani 137,782.49 za bidhaa zenye thamani ya takriban TZS 1,280,492,887.00 ziliteketezwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

## 2.3 KUBORESHA HUDUMA ZA MAABARA

Maabara ya TFDA ilianzishwa chini ya kifungu 14(1) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 ili kufanya uchunguzi wa sampuli za chakula, dawa, vifaa tiba, vipodozi, malighafi za kutengenezea bidhaa hizo, vifungashio na vitendanishi pamoja na kufanya tafiti na mafunzo.

### 2.3.1 Uchunguzi wa sampuli

Kulikuwa na jumla ya sampuli 5,067 za chakula, dawa, vifaa tiba na vipodozi, ambapo sampuli 3,474 zilizopokelewa Maabara ya TFDA Dar es salaam, sampuli 730 maabara ya TFDA Kanda ya Ziwa, Mwanza na sampuli 863 kutoka vituo vyenye maabara hamishika. Sampuli zote zilizokuwepo zilifanyiwa uchunguzi ambapo sampuli 4,580 (90%) zilifaulu. Mchanganuo wa uchunguzi wa sampuli umeainishwa katika vipengele (2.3.1.1 - 2.3.1.4).

#### 2.3.1.1 Sampuli za dawa

Jumla ya sampuli 797 za dawa zilizopokelewa katika maabara ya Dar es Salaam (677), maabara ya Kanda ya Ziwa (120) na sampuli 863 kutoka vituo vya maabara hamishika. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18 sampuli 158 zilibaki bila kufanyiwa uchunguzi na hivyo kupelekea sampuli zilizohitaji kuchunguzwa kuwa 1,818 ambapo sampuli zote zilichunguzwa na 1,808 (99%) zilikidhi vigezo kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.15

**edwali Na.15 Uchunguzi wa sampuli za Dawa**

| Chanzo cha sampuli | Baki (2017/18) | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Faulu | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Idadi | % |
| Ukaguzi-dawa za binadamu | 5 | 38 | 43 | 43 | 43 | 100 |

| Chanzo cha sampuli | Baki (2017/18) | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Faulu | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Idadi | % |
| Ufuatiliaji katika soko (PMS) | 23 | 110 | 133 | 133 | 133 | 100 |
| Wateja wa nje | 37 | 17 | 54 | 54 | 54 | 100 |
| Uchunguzi wa awali | 93 | 1,405 | 1,498 | 1,498 | 1,488 | 99 |
| *Miscellaneous* | 0 | 6 | 6 | 6 | 6 | 100 |
| Sampuli za kujipima umahiri (PT) | 0 | 25 | 25 | 25 | 25 | 100 |
| Dawa za Utafiti | 0 | 59 | 59 | 59 | 59 | 100 |
| **Jumla** | **158** | **1,660** | **1,818** | **1,818** | **1,808** | **99** |

#### 2.3.1.2 Sampuli za chakula

Jumla ya sampuli 2,246 za chakula zilipokelewa ikiwa ni pamoja na sampuli 610 kutoka maabara ya Kanda ya Ziwa. Sampuli 233 zilikuwa baki kutoka mwaka wa fedha 2017/18 na hivyo kufanya jumla ya sampuli zilizohitaji kuchunguzwa kuwa 2,479. Sampuli zote zilichunguzwa ambapo sampuli 2,041 (82%) zilikidhi vigezo kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.16.

**Jedwali Na.16: Uchunguzi wa sampuli za Chakula**

| Chanzo cha sampuli | Baki (2017/18) | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Faulu | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Idadi | % |
| Usajili | 60 | 702 | 762 | 762 | 624 | 82 |
| Ukaguzi | 127 | 653 | 780 | 780 | 617 | 79 |
| Ufuatiliaji katika soko (PMS) | 32 | 606 | 638 | 638 | 540 | 86 |
| Wateja wa nje | 3 | 173 | 176 | 176 | 137 | 78 |
| Sampuli za utafiti | 5 | 33 | 38 | 38 | 38 | 78 |
| Sampuli za kujipima umahiri (PT) | 6 | 79 | 85 | 85 | 85 | 78 |
| **Jumla** | **233** | **2,246** | **2,479** | **2,479** | **2,041** | **82** |

#### 2.3.1.3 Uchunguzi wa sampuli za vifaa tiba na vitendanishi

Jumla ya sampuli 126 za vifaa tiba na 59 za vitendanishi zilipokelewa. Vilevile, sampuli 89 za vifaa tiba zilikuwa ni baki ya mwaka 2017/18 na hivyo kupelekea sampuli zilizohitaji kuchunguzwa kuwa 274. Sampuli zote 215 za vifaa tiba zilichunguzwa ambapo 210 (98%) zilikidhi vigezo. Aidha, sampuli zote 59 za vitendanishi zilizochunguzwa zilikidhi vigezo kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.17.

**Jedwali Na.17: Uchunguzi wa sampuli za vifaa tiba na vitendanishi**

| Bidhaa | Chanzo cha sampuli | Baki 2017/18 | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Faulu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Idadi | % |
| Vifaa tiba | Ukaguzi | 0 | 32 | 32 | 32 | 27 | 84 |
| | Ufuatiliaji katika soko (PMS) | 89 | 59 | 148 | 148 | 148 | 100 |
| | Wateja wa nje | 0 | 7 | 7 | 7 | 7 | 100 |
| | Sampuli za kujipima umahiri (PT) | 0 | 28 | 28 | 28 | 28 | 100 |
| | **Jumla ndogo** | **89** | **126** | **215** | **215** | **210** | **98** |
| Vitendanishi | Ukaguzi | 0 | 57 | 57 | 57 | 57 | 100 |
| | Wateja wa nje | 0 | 2 | 2 | 2 | 2 | 100 |
| **Jumla ndogo** | | **0** | **59** | **59** | **59** | **59** | **100** |
| | **Jumla Kuu** | **89** | **185** | **274** | **274** | **269** | **98** |

### 2.3.1.4 Sampuli za vipodozi

**2.3.1.4 Sampuli za vipodozi**
Jumla ya sampuli 321 za vipodozi zilipokelewa. Aidha, sampuli 175 zilikuwa ni baki ya mwaka 2017/18 na hivyo kufanya jumla ya sampuli zilizohitaji kuchunguza kuwa 496. Sampuli zote zilichunguzwa na zote zilikidhi vigezo kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.18.

**Jedwali Na.18: Mchanganuo wa Uchunguzi wa sampuli za Vipodozi**

| Chanzo cha sampuli | Baki (2017/18) | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Faulu | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Faulu | % |
| Usajili | 1 | 41 | 42 | 42 | 36 | 86 |
| Ukaguzi | 0 | 69 | 69 | 69 | 45 | 65 |
| Ufuatiliaji katika soko (PMS) | 173 | 205 | 378 | 378 | 374 | 99 |
| Wateja wa nje | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 100 |
| Uchunguzi wa awali | 0 | 6 | 6 | 6 | 6 | 100 |
| **Jumla** | **175** | **321** | **496** | **496** | **462** | **93** |

### 2.3.2 Utekelezaji wa mifumo ya maabara kwa viwango vya ISO/IEC 17025 na WHO/GLP

Mamlaka iliendelea kuimarisha mifumo ya maabara ambapo ilifanyiwa ukaguzi wa nje na Shirika la Afya Dunia (WHO) kwa maabara za dawa na maikrobaiologia ambapo upungufu uliobainika katika ukaguzi huo unafanyiwa kazi. Hata hivyo, TFDA inaendelea kushikilia cheti cha Ithibati cha ISO/IEC:17025 pamoja na WHO/GLP.

## 2.4 KUIMARISHA UTOAJI ELIMU KWA UMMA NA KUBORESHA HUDUMA KWA WATEJA

Utoaji wa elimu kwa umma na huduma kwa wateja inalenga kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi juu ya kazi na majukumu ya TFDA, mahitaji ya Sheria sanjari na kujengewa uelewa wa taratibu za kuanzisha biashara ili kukidhi vigezo vya usalama na ubora wa bidhaa zinazodhibitiwa.

### 2.4.1 Elimu kwa umma

Elimu kwa umma husaidia kuongeza uelewa kwa watumiaji wa bidhaa katika kuhakikisha matumizi sahihi ya bidhaa pamoja na kuongeza utii wa sheria bila shuruti. Kazi za uelimishaji umma zilizotekelezwa katika kipindi hiki zimeainishwa katika Jedwali Na.19.

**Jedwali Na. 19: Njia zilizotumika kuelimisha jamii**

| Na | Kazi | Idadi | Maelezo/Maoni |
|---|---|---|---|
| 1. | Kutoa elimu kwa njia ya mihadhara | 58 | Jumla ya washiriki 39,073 ambao ni wanafunzi, waalimu na vikundi vya wajasiriamali wanaojihusisha na bidhaa zinazodhibitiwa na TFDA kutoka shule 46, Wilaya za Urambo, Karagwe, Kyerwa, Mvomero, Madaba, Manispaa ya Songea, Kisarawe na Handeni pamoja na wafanyabiashara wa vipodozi wa mkoa wa Dar es salaam walifikiwa na kupatiwa elimu kuhusu matumizi sahihi ya dawa na vipodozi. |
| 2. | Kushiriki maonesho | 11 | Mamlaka ilishiriki katika maonesho mbalimbali kulingana mialiko ya kushiriki maonesho hayo iliyopokelewa ikiwemo maonesho ya wiki ya utumishi wa Umma barani Afrika yaliyofanyika Nairobi ambapo TFDA ilishinda tuzo ya taasisi yenye mifumo bora ya utoaji huduma kwa wananchi. |
